

TANGAZO

WIZARA YA ARDHI KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA INAFANYA ZOEZI LA UHAKIKI WA ULIPAJI WA KODI YA PANGO LA ARDHI KWA WAMILIKI WOTE WA ARDHI KATIKA WILAYA YA NACHINGWEA.

KWA MUJIBU WA **SHERIA YA ARDHI NA. 4 YA MWAKA 1999 FUNGU LA 33**, TAASISI ZA UMMA, MAKAMPUNI AU MTU MMOJA MMOJA WANAOMILIKI VIWANJA AU MASHAMBA WANATAKIWA KULIPA KODI YA PANGO LA ARDHI KILA MWAKA.

WIZARA YA ARDHI INAWATAKA WAMILIKI WOTE WA ARDHI AMBAO HAWAJALIPA, KULIPA KODI YA PANGO LA ARDHI KABLA YA TAREHE 31/03/2018 VINGINEVYO HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAO IKIWA NI PAMOJA NA KUFIKISHWA MAHAKAMANI AU **KUFUTIWA HAKI YA KUMILIKI** ARDHI ZAO KWA MUJIBU WA SHERIA.

AIDHA, ILI KUEPUKA USUMBUFU UTAKAOJITokeza WAMILIKI AMBAO WAMELIPIA KODI YA ARDHI HADI MWEZI JUNI 2018 WANAHIMIZWA KUACHA NAKALA ZA NYARAKA ZAO ZA UMILIKI PAMOJA NA RISITI ZA MALIPO YA KODI WALIZOFANYA MAJUMBANI MWAO KWANI TUTAPITA KUKAGUA NYUMBA HADI NYUMBA.

Tangazo hili limetolewa na:-

KATIBU MKUU

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI